Ombi la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam ("DAWASA") la Kurekebisha Bei ya Huduma za Maji lililowasilishwa Tarehe 11 Machi, 2009

Agizo Namba 09-008

1.0 UTANGULIZI

Tarehe 11 Machi, 2009 Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma ya Maji na Nishati ("EWURA") ilipokea ombi la Mamlaka ya Majisafi na Majitaka ya Dar-es-Salaam ("DAWASA") la kutaka kuongeza bei ya huduma ya majisafi kwa asilimia 34.3% na ile ya majitaka kwa asilimia 30.4%. Katika ombi hilo, DAWASA ilipendekeza bei hizo zianze kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Mei, 2009. Kulingana na DAWASA, madhumuni ya kuomba marekebisho hayo ya bei kunatokana na ongezeko la gharama ya kutoa huduma ya majisafi na majitaka, mahitaji ya kulipia mchango wa DAWASA kwenye mradi wa Majisafi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam pamoja na kulipa deni. Mabadiliko ya bei yalifanyika kwa mara ya mwisho Julai 2006 ambapo bei ya huduma ya majisafi ilipanda kwa asilimia 35.9 kwa wateja wa kundi la kwanza ("Band 1"), na asilimia 29.2 kwa kundi la pili ("Band 2"). Vile vile bei ya majitaka ilipanda kwa asilimia 19.

Kulingana na kifungu cha 50 cha sheria iliyounda EWURA, (Energy and Water Utilities Regulatory Authority Act, Cap 414), tathmini kuhusiana na maombi ya DAWASA, pamoja na mambo mengine, imezingatia masharti ya "Mkataba wa Ukodishaji" kati ya DAWASA *("mkodishaji")* na "Dar es Salaam Water and Sewerage Corporation ("DAWASCO"), *("mwendeshaji"),* uliotiwa saini tarehe 12 Desemba, 2005. Mkataba huo unaainisha utaratibu utakaotumika katika kushughulikia maombi ya marekebisho ya gharama za huduma za majisafi na majitaka.

2.0 MAONI YA WADAU

Mnamo tarehe 27 Mei 2009, EWURA ilifanya taftishi kwenye ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam na tarehe 28 Mei 2009, kwenye ukumbi wa Mkoani, Kibaha kama sehemu ya kupata maoni kutoka kwa wadau kuhusu uhalali wa ombi hilo la kuongeza bei za huduma za majisafi na majitaka. Hoja za Baraza la Watumiaji Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (CCC) zilihusu maeneo machache yanayopata huduma ya majisafi na majitaka; kiwango kikubwa cha upotevu wa maji; ufanisi mdogo wa kukusanya mapato na muundo wa DAWASA na DAWASCO ambao unamwongezea mzigo mteja wa maji. Hoja za Baraza la Ushauri la Serikali (Government Consultative Council - GCC) zilihusu ufanisi mdogo wa kukusanya mapato na miundombinu iliyochakaa. Wadau wengine walihoji pia kiwango kidogo cha sehemu zinazopata huduma ya majisafi na majitaka; kiwango kikubwa cha upotevu wa maji; ufanisi mdogo wa kukusanya mapato na uwezo wa wananchi kulipia ongezeko la bei ya maji na huduma mbaya kwa wateja. Maoni ya wadau yamezingatiwa katika kufikia maamuzi kuhusu maombi ya DAWASA ya kuongeza bei ya maji.

3.0 MATOKEO MUHIMU YA UCHAMBUZI

(i) Mkataba wa Ukodishaji unaainisha kuwa mchakato wa urekebishaji bei za maji wa DAWASA utazingatia Kanuni ya Kimahesabu ya Kurekebisha Bei (“Indexation Formula”) iliyowekwa kwenye mkataba huo. DAWASA imekokotoa kwa usahihi mabadiliko ya kiuchumi katika kanuni hiyo ya kimahesabu ili kufikia mapendekezo ya bei, isipokuwa bei ya maji kwa ajili ya mkodishaji (“water lessor tariff”) na bei kwa ajili ya kulipia maunganisho mapya kwa ajili ya wateja wa nyumbani (“ FTDWSCF tariff”);.

(ii) Mapendekezo ya bei ya huduma za majisafi kama yalivyokokotolewa kwa kutumia Kanuni ya Kimahesabu ya Kurekebisha Bei (“Indexation Formula”) yanaweza kuipatia DAWASA mapato yanayoweza kukidhi asilimia 92 ya mahitaji. Ili kutathmini kama bei itokanayo na ukokokotoaji wa Kanuni ya Kimahesabu ya Kurekebisha Bei (“Indexation Formula”) inatosheleza

mahitaji, mfumo wa kukokotoa bei ya huduma ya majisafi na majitaka utapitiwa upya katika mwaka 2009/2010;

(iii) Ongezeko la wateja waliofungiwa dira za maji utaiwezesha DAWASA kupima kwa usahihi zaidi maji inayoyauza na wateja wa majisafi na majitaka wataweza kulipia ankara zao kulingana na matumizi halisi ya maji;na

(iv) Uboreshaji wa huduma kwa wateja utaongeza utashi wa kulipia huduma ya majisafi na majitaka.

4.0 UAMUZI

Kutokana na hoja zilizotolewa na DAWASA kuelezea uhalali wa maombi yao, maoni yaliyotolewa na wadau na tathmini iliyofanywa, EWURA imeona kuwa ombi la nyongeza za bei lina mantiki na ni halali.

Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA katika kikao chake cha tarehe 10 Julai, 2009 ilijadili ombi la DAWASA na kutoa maamuzi yafuatayo:

4.1 Bodi imeidhinisha ongezeko la asilimia 30 ya bei ya majisafi na asilimia 30.4 ya bei ya majitaka. Bei zilizoidhinishwa zinaonyeshwa kwenye jedwali Na 1, 2 na 3 hapa chini.

Jedwali 1: Bei za Majisafi na Majitaka Zilizoidhinishwa

Aina ya Bei	**Bei ya Sasa (TZS / Mita ya Ujazo)**	**Bei Iliyoombwa (TZS / Mita ya Ujazo)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS / Mita ya Ujazo)**
Majisafi			
Gharama ya Mwendeshaji	488	637	637
Gharama ya Kuunganisha Huduma ya Maji Katika Makazi kwa Mara ya Kwanza	29	43	37
Gharama ya Mkodishaji	137	198	176
Jumla ya Bei kwa Mteja	**654**	**878**	**850**
Majitaka			
Gharama ya Mwendeshaji	133	174	174
Gharama ya Mkodishaji	41	53	53
Jumla ya Bei kwa Mteja	**174**	**227**	**227**

Jedwali 2: Mpangilio wa Bei Zilizoidhinishwa

	Bei ya Sasa (TZS / Mita ya Ujazo)	**Bei Iliyoombwa (TZS / Mita ya Ujazo)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS / Mita ya Ujazo)**
Bei ya Majisafi			
Band 1: kwa matumizi hadi $5m^3$ kwa mwezi kwa watumiaji wa majumbani na maghati.	488	637	637
Band 2: kwa matumizi yatakayozidi $5m^3$ kwa mwezi kwa watumiaji wa majumbani na wasio wa majumbani.	654	878	850
Bei ya Majitaka	174	227	227

Jedwali 3:Bei ya Maji Iliyoidhinishwa kwa Wateja wa Nyumbani Wasio na Dira kwa Mwezi.

Eneo	**Makadirio ya Matumizi ya Maji ya Sasa (m^3)**	**Bei ya sasa, TZS/Mwezi**	**Makadirio ya Matumizi ya Maji Yaliyoidhinishwa (m^3)**	**Bei Iliyoidhinishwa TZS/Mwezi**
Bagamoyo	31	20,274.00	32	26,135.00
Boko	52	34,008.00	41	33,785.00
Kawe	52	34,008.00	41	33,785.00
Kinondoni	43	28,122.00	45	37,185.00
City Centre	52	34,008.00	35	28,685.00
Ilala	36	23,544.00	35	28,685.00
Magomeni	36	23,544.00	36	29,535.00
Kibaha	43	28,122.00	43	35,485.00
Kimara	36	23,544.00	36	29,535.00
Tabata	20	13,080.00	20	15,935.00
Temeke	43	28,122.00	35	28,685.00

4.2 Ifikapo tarehe 30 Juni 2010 au kabla ya hapo, DAWASA inatakiwa;

4.2.1 kupitia gharama za Mwendeshaji na Kanuni za Kimahesabu ya Kurekebisha Bei ("*Indexation formula"*) kwa kujumuisha mabadiliko na mwenendo wa kiuchumi na hali ya kiufundi *("technical conditions"*) na masharti mengine kama yalivyoainishwa katika Kifungu Na. 40.1(a) cha Mkataba wa Ukodishaji: na

4.2.2 kupitia malengo ya kiutendaji yaliyo kwenye Mkataba wa Ukodishaji, kwa kiwango kitakachoridhiwa na EWURA.

4.3 Ifikapo tarehe 31 Januari 2010 au kabla ya hapo, DAWASA inatakiwa;

4.3.1 kuongeza idadi ya wateja waliofungiwa dira za maji kutoka 39,000 hadi 104,000 ambapo wateja wote wa Kimara, Kibaha,Kati Kati ya Jiji na Boko wanapaswa kuwa wamefungiwa dira za maji: na

4.3.2 kupitia Kanuni za Utendaji ("Codes of Practice") kama ilivyoelekezwa kwenye Kifungu Na. 13 cha Mkataba wa Ukodishaji kati ya DAWASA na DAWASCO.

4.4 Ifikapo tarehe 31 Desemba 2009 au kabla ya hapo, DAWASA inatakiwa kuwasilisha EWURA mpango wake wa kupunguza maji yanayopotea kutoka asilimia 53 ya sasa hadi chini ya asilimia 35 ifikapo tarehe 31 Desemba 2013.

4.5 DAWASA inatakiwa kupunguza kiasi cha maji yanayopotea kutoka asilimia 53 ya sasa hadi asilimia 40 ifikapo Juni 2010, kama ilivyoanishwa kwenye bajeti ya DAWASCO ya 2009/2010, na kiwango hiki kitachukuliwa kama kimefikiwa kwa marekebisho yote ya bei yatakayofanyika baada ya tarehe 30 Juni 2010.

4.6 Ifikapo tarehe 31 Desemba 2009 au kabla ya hapo, DAWASA inatakiwa iwe imetoa uthibitisho wa kutosha wa jinsi inavyotekeleza mpango wake wa kuimarisha mahusiano, mawasiliano, utoaji habari, na uelimishaji wa wateja. Taarifa ya utekelezaji wa mpango huo iwasilishwe EWURA katika kila ripoti yake ya mwaka. EWURA itazingatia taatifa hiyo wakati wa kufanya tathmini ya uhalali wa maombi ya bei.

4.7 DAWASA itaendelea kuwasilisha kwa EWURA taarifa zake za fedha na za utendaji kwa mujibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa DAWASA ikilinganishwa na vyombo vingine vya utoaji wa huduma za maji na uboreshaji wa huduma zake. EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yatakayowasilishwa na DAWASA katika siku zijazo. Pia DAWASA inatakiwa kuhakikisha kwamba taarifa zinazotolewa katika ripoti za kila mwezi zinaboreshwa.

Agizo hili litaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Agosti 2009.

Simon F. Sayore
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
EWURA

Haruna Masebu
Mkurugenzi Mkuu
EWURA

Dar-es-Salaam 25 Julai 2009